JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI

(RUWASA)

# MWONGOZO WA UPANGAJI BEI YA MAJI

**SEPTEMBA, 2022**




# Mwongozo wa Upangaji Bei

RUWASA
Rural Water Supply and Sanitation Agency
"Maji Bombani"

Benki ya NBC,Tawi la Mazengo, Barabara Kuu,
S. L. P 412, 40473 DODOMA.
Simu: +255 2323563/4
Barua Pepe: dg@ruwasa.go.tz

# YALIYOMO


YALIYOMO.....2
SEHEMU YA KWANZA.....3
1.0 UTANGULIZI.....3
1.1 Usuli.....3
2.0 UPANGAJI WA BEI ZA MAJI NA NJIA ZA KUKUSANYA MAUZO YA MAJI.....5
2.1 Maana ya Bei ya Maji.....5
2.2 Mchakato wa Kuamua na Kuidhinisha Bei ya Maji.....5
2.3 Makisio ya Mahitaji ya Fedha Gharama za Uendeshaji na Uendelezaji wa Huduma.....8
2.3.1 Makisio ya Gharama za Uendeshaji na Matengenezo (O&M Costs).....9
2.3.2 Makisio ya Gharama za Uchakavu (Depreciation Expenses).....10
2.3.3 Makisio ya Gharama za Uwekezaji.....11
2.3.4 Bei kwa Makundi Mbali Mbali ya Watumiaji wa Maji.....12
2.4 Makisio ya Bei ya Maji.....12
2.4.1 Gharama za Kukidhi Uendeshaji wa Chombo (full cost recovery).....12
2.4.2 Makisio ya Mapato na Uchambuzi wa Bei ya Maji.....13
2.4.4 Kuoanisha Bei ya Maji na Uwezo wa Kulipa.....14
2.4.3 Bei kwa Makundi Mbali Mbali ya Watumiaji wa Maji.....14
2.4.5 Mapendekezo ya Bei ya Maji.....15
3.0 MAPITIO YA MWONGOZO.....15

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1. Usuli

Dhana ya Jumuiya za Huduma ya Maji ngazi ya jamii imejengwa katika msingi kuwa jamii itakuwa sehemu ya mipango, maamuzi, ujenzi na uendeshaji wa mfumo wa huduma za maji katika maeneo yao, ili kuhakikisha kuwa mfumo mzima wa miundombinu na huduma za maji zinakuwa endelevu. Kiuhalisia, mafanikio ya ushirikishaji wa jamii yanatarajiwa yaonekane katika kiwango chao cha umiliki, uwajibikaji na katika uendeshaji wa huduma. Umiliki na uwajibikaji unapimwa kwa utayari wa jamii kutumia rasilimali muda, nguvu na fedha katika kuendesha, kulinda na kuendeleza huduma katika maeneo yao.

Dhana hii inaakisi matakwa ya Sera ya Maji (NAWAPO) ya mwaka 2002 na ina nguvu ya kisheria kwa mujibu ya Kifungu cha 33. (1) (b) na (e); na Kifungu cha 38. (a), (b) and (c) vya Sheria ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Na.5 ya Mwaka 2019. Vifungu hivi vinatoa mamlaka kwa Jumuiya za Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii kuendesha huduma kutoza huduma ya maji na kukusanya maduhuli.

Kifungu cha 26 (1) na (2) cha Kanuni ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira (Usajili na Uendeshaji) ya mwaka 2019 inazitaka jumuiya kuwasilisha mapendekezo ya bei za maji kulingana na mwongozo utakaoandaliwa na RUWASA. Mapendekezo ya bei yatawasilishwa RUWASA kwa ajili ya uchambuzi wa kina na kupata idhini ya Bodi ya RUWASA.

Ingawa sheria imetoa mamlaka ya kutoza bei katika huduma ya maji kwa watumaiji wa huduma hizo, bado kuna Jumuiya ambazo hazitozi kabisa huduma ya maji na zipo Jumuiya zinatoza kiwango ambacho kinatumika chote kwenye gharama

za kukusanya tozo yenyewe. Hata Jumuiya zinazotoza, kiwango cha tozo kinapangwa kwa makadirio au kinaigwa kutoka kwenye Jumuiya nyingine ambazo tayari zina utaratibu wa kutoza huduma. Uhalisia ni kuwa, kwenye Jumuiya nyingi, upangaji na utozaji wa huduma ya maji hufanywa na Jumuiya bila kuzingatia vigezo vyovyote vilivyowekwa na mamlaka za usimamizi.

Mwongozo huu umetolewa kwa ajili ay kutumika na kuzingatiwa na Jumuiya zote nchi nzima katika mchakato wa kupanga bei, kutoza na kusimamia maduhuli ya maji yanayoweza kukidhi gharama za uendeshaji, matengenezo na uchakavu.

## 1.2. Lengo

Lengo kuu la mwongozo huu ni kutoa maelekezo ya namna bora ya kusimamia upangaji wa bei na usimamizi wa fedha za maduhuli ya maji, ili kuifanya miradi ya maji vijijini kuwa endelevu. Mwongozo huu utatumiwa na Jumuiya za Utoaji wa Huduma ya Maji ngazi ya Jamii.

### Malengo Mahsusi

i. Namna ya kukokotoa bei ya maji;

ii. Kueleza maana ya makusanyo ya fedha za maji;

iii. Kuelewa na kuchagua njia bora ya kukusanya fedha za Jumuiya;

iv. Kuandaa bajeti ya jumuiya ya maji katika maeneo yao;

v. Kuelewa matumizi sahihi ya fedha za makusanyo ya maji;

vi. Kutunza kumbukumbu za mapato na matumizi;

vii. Kuelewa utunzaji wa fedha taslimu na taratibu za kibenki na taasisi nyingine; na

viii. Kuandaa taarifa ya mapato na matumizi, Mfano; Mwezi, Robo au Mwaka.

# 2.0 UPANGAJI WA BEI ZA MAJI NA NJIA ZA KUKUSANYA MAUZO YA MAJI

## 2.1 Maana ya Bei ya Maji

Bei ya maji ni tozo iliyopangwa kwa ajili ya kulipwa na watumiaji maji kulingana na matumizi ya maji ili kukidhi gharama za uendeshaji na matengenezo.

## 2.2 Mchakato wa Kuamua na Kuidhinisha Bei ya Maji

Bei ya maji ina mchango mkubwa katika mnyororo mzima wa kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji na kuimarisha ubora na uendelevu wa huduma inayotolewa. Kwa mantiki hiyo, bei inayopangwa na kuidhinishwa kutumika ni muhimu iwe inakidhi vigezo vya kiuchumi, kisosholojia na kiutawala. Mchakato mzima wa upangaji, uamuzi na uidhinishaji wa bei ya maji utakuwa kama ifuatavyo:

2.2.1 Kiongozi wa Timu ya Utendaji ataanzisha mchakato wa mabadiliko ya bei kwa kuandaa mpango biashara wa miaka mitatu na atashirikiana na Meneja wa Wilaya wa RUWASA na Mkurugenzi wa Halmashauri wa eneo husika baada ya kujiridhisha kuwa mabadiliko ya bei yatasaidia katika kuimarisha ubora na uendelevu wa huduma;

2.2.2 Meneja wa RUWASA Wilaya na Mkurugenzi wa Halmashauri katika eneo husika la huduma watafanya kazi na kuisaidia Timu ya Uendeshaji kuzingatia Mwongozo wa kuandaa mpango biashara wa miaka mitatu na Mwongozo wa ukokotoaji wa bei za maji kwa wateja wa Virula/Vichoteo na binafsi/majumbani;

2.2.3 Baada ya kukamilisha zoezi la maandalizi ya mpango biashara na ukokotoaji wa bei, Timu ya Uendeshaji kwa kushirikiana na RUWASA na Halmashauri husika, watawasilisha taarifa kwenye Kamati ya Maji ili kuwa na uelewa wa pamoja

na kupata idhini ya kuendelea na mchakato wa mabadiliko ya bei;

2.2.4 Mwenyekiti wa Kamati wakishirikiana na RUWASA na Halmashauri, watatembelea na kufanya vikao na viongozi wa juu wa eneo la hudumakatika ngazi ya Kijiji na Kata ili kuelezea, kuelewesha na kutoa taarifa ya maudhui na maendeleo ya mchakato wa mabadiliko na hatua zinazofuata;

2.2.5 Kamati ya Maji itamwandikia rasmi Meneja wa RUWASA katika Wilaya husika maombi ya kubadilisha bei ya maji. Meneja wa Wilaya atamtaarifu Meneja wa Mkoa RUWASA kuhusu maombi husika na kutoa maoni na ushauri wake juu ya umuhimu na uhalali wa maombi husika;

2.2.6 Meneja wa RUWASA Mkoa ataunda timu ya watu wasiozidi watano na wasiopungua watatu kwa ajili ya kufanya tathmini ya bei. Baada ya tathmini kukamilika timu itawasilisha kwa Meneja wa RUWASA Mkoa taarifa ya tathmini (timu hiyo ihusishe wataalam kutoka kada zifuatazo Uhandisi, Uhasibu, Uchumi, Maendeleo ya Jamii);

2.2.7 Meneja wa Mkoa RUWASA ataitisha kikao cha wadau wa huduma ya maji katika eneo ambalo Chombo kimeomba mabadiliko ya bei kwa lengo ya kupata maoni kuhusu maombi yaliyowasilishwa na Kamati ya Maji;

2.2.8 Meneja wa Wilaya kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya Vijiji/Kijiji na Kamati ya Maji wataratibu maandalizi ya kikao husika ambacho kitaitishwa na Meneja wa RUWASA Mkoa katika eneo husika ambapo wajumbe watakuwa wananchi wote wanufaika wa huduma na wadau wote muhimu katika eneo la huduma. Taarifa na agenda za kikao zitatangazwa angalau siku tano kabla ya Kikao ili kutoa nafasi ya maandalizi na ushiriki wenye tija;

2.2.9 Mwenyekiti wa kikao cha wadau cha kupokea maoni atakuwa Meneja wa RUWASA Mkoa na Katibu atakuwa Meneja wa Wilaya kwa kushirikina na Timu ya Uendeshaji;

2.2.10 Baada ya kufungua kikao, Mwenyekiti atawakaribisha viongozi wa Serikali ngazi ya Kata na Kijiji ambao ndio watakaoelezea Agenda kuu ya kikao kabla ya kuwakaribisha Kamati ya Maji kuwasilisha hoja na kutoa maelezo ya ufafanuzi ikisaidiwa na Meneja wa RUWASA na Mkurugenzi wa Halmashauri katika eneo husika;

2.2.11 Wajumbe wa Mkutano watapewa nafasi ya kutosha kuhoji, kutoa mrejesho na kutoa mawazo yao kwa mpangilio na nidhamu ya kikao. Maoni na masuala yote katika kikao yatawekwa katika maandishi na yatakuwa sehemu ya muhtasari wa kikao;

2.2.12 Ikitokea kuna hoja hazikupata ufafanuzi wa kina katika kikao hicho, Chombo kitapewa muda wa siku zisizozidi 7 baada ya kikao kufanyika kujibu kwa maandishi na kuwasilisha kwa meneja RUWASA wa Mkoa kupitia kwa Meneja RUWASA Wilaya;

2.2.13 Baada ya hoja zote kujibiwa, Meneja wa Mkoa atajiridhisha na mapendekezo ya bei kwa kuanisha na maoni ya wadau na ataandika barua ya maombi ya kuidhinisha matumizi ya bei kwa Mkurugenzi Mkuu. Barua itaambatishwa na muhtasali wa kikao cha maoni ya wadau, orodha ya hoja zilizoibuliwa na kujibiwa, mpango biashara wa miaka mitatu wa chombo, taarifa ya tathmini ya bei ya timu ya tathminini kama ilivyoainishwa katika kipengele 2.2.6;

2.2.14 Mapendekezo ya Maombi yaliyowasilishwa na RUWASA MKoa yatafanyiwa mapitio na Kamati Maalum itakayoteuliwa na Mkurugenzi Mkuu na yatajadiliwa katika kikao cha menejimenti ya RUWASA na kupelekwa kwenye kikao cha Bodi kwa ajili ya kupata idhini. Bei ikishaidhinishwa, Mkurugenzi

Mkuu atatoa tangazo la bei katika gazeti la Serikali na kuwajulisha Chombo husika juu ya bei zilizoidhinishwa zikiwa na masharti ya matumizi ya bei ("Tariff Condition Order"), nakala ya barua atapewa Meneja wa RUWASA Mkoa na Wilaya wa Chombo husika; na

2.2.15 Kamati ya Maji itatoa taarifa na kuwatangazia wananchi wa eneo la huduma kuhusu tarehe rasmi ya kuanza kutumika kwa bei iliyoidhinishwa. Taarifa zitasambazwa katika mbao za matangazo na maeneo muhimu ya mikusanyiko kwa urahisi wa kuwafikia walengwa.

## 2.3 Makisio ya Mahitaji ya Fedha Gharama za Uendeshaji na Uendelezaji wa Huduma

Makadirio ya mahitaji ya fedha kwa ajili ya kulipia gharama za uendeshaji na uendelezaji wa skimu /chombo yatatokana mchanganuo uliopo kwenye Mpango wa Kibiashara (Business Plan) wa Chombo husika. Mahitaji ya fedha za kutosheleza kulipia gharama zote za uendeshaji na uwekezaji katika kuboresha huduma ya maji yanapatikana kwa kujumlisha gharama za makundi makundi makubwa matatu (3), kama ifuatavyo:

**Jumla ya Mahitaji ya Fedha = O + M + I**

**Ambapo:**

O&M = Gharama ya Uendeshaji na Matengenezo (Operational & Maint. Costs)

M = Gharama za Uchakavu wa Miundombinu na Mitambo (Depreciation Costs)

I = Gharama ya Uwekezaji (rehabilitation, replacement and new investment)

### 2.3.1 Makisio ya Gharama za Uendeshaji na Matengenezo (O&M Costs)

Makisio ya gharama ya uendeshaji na matengenezo kwa miaka mitatu yatatokana na uchaambuzi uliofanyika katika Jedwali Na. 1 na kwa kulinganisha na gharama zilizotumika katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita. Chombo kinaweza kuongeza makundi au aina ya matumizi kwa jinsi kinavyoendesha shughuli zake.

**Jedwali Na. 1 Makisio ya Gharama za Uendeshaji na Matengenezo**

| Aina ya Matumizi | Gharama (TZS) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | M-3 | M-2 | M-1 | Mwaka wa sasa (M) | M+1 | M+2 | M+3 |
| | | | | | | | |
| **Uzalishaji Maji** | | | | | | | |
| Umeme | | | | | | | |
| Madawa | | | | | | | |
| Mafuta na Vilainisho (Generator) | | | | | | | |
| Kutumia Maji (Water User Fee) | | | | | | | |
| Maabara | | | | | | | |
| Utunzaji wa Chanzo/Vyanzo vya Maji | | | | | | | |
| Kukunua maji kwa Ujumla | | | | | | | |
| Jumla ya Gharama za Uzalishaji | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| **Gharama za Usambazaji** | | | | | | | |
| Umeme wa Pampu (Booster Pumps) | | | | | | | |
| Mafuta na Vilainisho vya Generator | | | | | | | |
| Ku test mita za wateja | | | | | | | |
| Jumla ya Gharama za Usambazaji | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| **Gharama za Matengenezo (Kutoka kwenye Jedwali…)** | | | | | | | |

| Aina ya Matumizi | Gharama (TZS) | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | M-3 | M-2 | M-1 | Mwaka wa sasa (M) | M+1 | M+2 | M+3 |
| Gharam za Watumishi | | | | | | | |
| Mshahara | | | | | | | |
| Malipo ya Vibarua | | | | | | | |
| Mcango wa Mifuo ya Pensheni | | | | | | | |
| llowances | | | | | | | |
| Jumla ya Gharama za Wafanyakazi | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| **Gharama za Utawala** | | | | | | | |
| Insurance | | | | | | | |
| Umeme wa Ofisi | | | | | | | |
| Posho ya Bodi | | | | | | | |
| Gharama ya Kukagua Hesabu | | | | | | | |
| Mafunzo ya Watumishi | | | | | | | |
| **Jumla ya Gharama za Utawala** | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| **Kuimarisha utoaji huduma (Busness Promoton)** | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| Uhusiano na mawasiliano na wateja (simu, internet nk) | | | | | | | |

### 2.3.2 Makisio ya Gharama za Uchakavu (Depreciation Expenses)

Gharama ya uchakavu wa miundombinu ni kwa ajili ya kukarabati miundombinu na gharama ya mtaji ni kwa ajili ya uwekezaji mpya. Ili kuweza kukokotoa gharama ya uchakavu na gharama za uwekezaji/mtaji inabidi thamani ya miundombinu (assets) pamoja na utaratibu wa kuanisha uchakavu wa "Assets" (depreciation Schedule) ufahamike. Kwa hali ya sasa hivi sio rahisi kwa Vyombo vya utoaji huduma za maji kijamii kuweza kumudu kupata tarifa zenye usahihi kuhusu thamani ya mali (assets) zao.

### 2.3.3 Makisio ya Gharama za Uwekezaji

Makisio ya gharama za uwekezaji ni kama yalivyowasilishwa katika Mpango wa uwekezaji katika kukarabati/kubadilisha miundombinu na uwekezaji mpya kama ulivyoainishwa katika Mpango wa Kibiashara. Mpango wa uwekezaji utakuwa na taarifa za Lengo la uwekezaji; Muhtasari wa uwekezaji unaolengwa; Kipindi cha usanifu na ujenzi; Gharam ya kila mwaka; na Chanzo cha fedha kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na: 2.**

**Jedwali Na. 2: Mpango wa Uwekezaji**

| Lengo la uwekezaji | Muhtasari wa Kazi Zitakazofanyika | Kipindi cha usanifu | Kipindi cha ujenzi | Mwaka-1 (Millioni TZS) | | Mwaka-2 (Millioni TZS) | | Mwaka-3 (Millioni TZS) | | Chanzo cha Fedha |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Uwekezaji | Ukarabati na Kubadilisha | Uwekezaji | Ukarabati na Kubadilisha | Uwekezaji | Ukarabati na Kubadilisha | |
| **Mfano:** Kuongeza kiasi cha maji yanayozalishwa kutoka Metaza ujazo……… hadi meta za ujazo…. | Kukarabati kisima (borehole) | 2 | 3 | | 10 | | | | | Chombo |
| | Kubadilisha pampu | 2 | 3 | | | | 15 | | | Chombo |
| | Kuchimba kisima kipya | 3 | 4 | 20 | | | | | | Chombo |
| | Kufunga pampu kwenye kisima Na. 3 | 2 | 3 | | | 30 | | | | Chombo |
| **Jumla Ndogo** | | | | **20** | **10** | **30** | **15** | **-** | **-** | |
| **JUMLA KUU TOTAL** | | | | | | | | | | |

Hata hivyo, makadirio ya fedha za uwekezaji yanaweza kuwa makubwa hivyo hivyo kupelekea ongezeko kubwa la be iza maji kwa mwaka mmoja. Ni muhimu kuzingatia uhimilivu wa gharama zinazoweza kubebwa na watumiaji maji.

### 2.3.4 Kanuni Mbadala ya Mahitaji ya Fedha

Kutokana na changamoto ya kupata taarifa sahihi na za kuaminika za thamani ya mali (asset value) kwenye vyombo vya maji kijamii, Chombo kitakokotoa mahitaji ya fedha za uendeshaji na uendelezaji wa huduma za maji kwa kutumia kanuni ifuatayo:

Kwa kanuni hii, Chombo kitatengeneza ratiba (roadmap) ya kuhakikisha mapato yake yanakua kuelekea kukidhi asilimia 150 (150%) ya gharama ya uendeshaji na matengezo. Kanuni hii ya ukokotoaji wa bei za maji inatumiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji ya  Kenya (WASREB) na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji Zambia (NWASCO). Kanuni hii imefikiwa baada ya utafiti wa muda mrefu walioufanya na ambaob ulibaini kanuni hiyo.

Kwa mantiki hiyo, Chombo kitakidhi 100% ya Gharama za Uendeshaji na matengenezo na 50% yake itakidhi gharama ya uchakavu (kwa ajili ya kukarabati miundombinu) na mtaji (kwa ajili ya uwekezaji).

## 2.4 Makisio ya Bei ya Maji

### 2.4.1 Gharama za Kukidhi Uendeshaji wa Chombo (full cost recovery)

Ili Chombo kiweze kukidhi mahitaji yake yote (full cost recovery) ya kuendesha shughuli za maji uwiano wa mapato na matumizi unapashwa kuwa kama ifuatavyo:

Mapato yatokanayo na Bei ya Maji (J) + Mapato Mengine (X) = Gharama za Uendeshaji na Matengenezo (Operation and

Maintenace Cost) + Uchakavu wa Miundo Mbinu (Depreciation) + Gharama za Uwekezaji/Mtaji (Return on Investment).

Mapato mengine yanaweza kutokana na:

a) Kurudisha maji yaliyokatwa;
b) Kuunga Maji; na
c) Msaada kutoka serikalini (subsidy).

Gharama ya uendeshaji na matengenezo inapatikana kwa mujibu wa **Jedwali Na. 1** na jumla ya gharama ya ukarabati na uwekezaji itapatikana kwa mujibu wa **Jedwali Na. 2** na isiwe zaidi ya 50% (ukomo) ya gharama ya uendeshaji na matengenezo.

### 2.4.2 Makisio ya Mapato na Uchambuzi wa Bei ya Maji

Mapato yanayopashwa kutokana na bei (mauzo) ya maji (J): (Gharama zote za uendeshaji chombo (A) – (Mapato mengine (X)). Makisio ya mapato yatakayotokana na bei (mauzo) ya maji na uchambuzi wa bei vimeonyeshwa kwenye Jedwali Na: 3 hapa chini.

**Jedwali Na. 3: Makisio ya Mapato na Uchambuzi wa Bei**

| Maelezo | Mwaka wa Sasa (M) | M+1 | M+2 | M+3 |
|---|---|---|---|---|
| Gharama za kukidhi uendeshaji wa Chombo (A) TZS | | | | |
| Mapato Mengine (X)TZS | | | | |
| Mapato yatakayotokana na bei ya maji (J)=(M-X) TZS | | | | |
| Maji yanayotegemewa kuzalishwa/mwaka (P) | | | | |
| Maji yatakayopotea (N)% | | | | |
| Maji yanayotegewa kufikia wateja (L)=P-N m3 | | | | |
| Wastani wa Bei ya maji (Q) =J/L TZS /m³ | | | | |

### 2.4.3 Bei kwa Makundi Mbali Mbali ya Watumiaji wa Maji

Ili kuanisha bei tofauti kwa makundi mbali mbali (differential tariff) ya watumiaji maji inabidi kutafuta uwiano wa matumizi ya maji kati ya makundi ili kuweza kutofautisha bei ya maji kati ya makundi hayo. **Jedwali Na: 4** inaonyesha mfano wa uwiano wa matumizi ya maji kwa makundi ya Viosk, Nyumbani, Taasisi na Biashara.

**Jedwali Na. 4: Uwiano wa Matumizi ya Maji kwa Makundi**

| Aina ya Matumizi | Uwiano wa Matumizi ya Maji kwa Makundi | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Mwaka wa Sasa | Mwaka 1 | Mwaka 2 | Mwaka 3 |
| Matumizi ya Vioski | 10.00% | 12.00% | | |
| Matumizi ya Nyumbani | 75.00% | 73.00% | | |
| Matumizi ya Taasisi | 15.00% | 13.00% | | |
| Matumizi ya Biashara | 5.00% | 2.00% | | |
| Jumla | 100.00% | 100.00% | | |

Kwa kutumia uwiano wa matumizi ya maji unaweza kuweka bei tofauti kwa makundi kwa mfano Viosk na matumizi ya nyumbani wanaweza kulipa chini ya wastani ambapo watafidiwa na makundi mengine kama biashara, taasisi ambayo yatalipa zaidi ya wastani maadam mapato yatakayotokana na mauzo ya maji yabaki vili vile.

Kwa wateja wasio na dira ya maji watalipa kwa kulingana na makadirio ya matumizi yao ukizidisha na bei ya kundi lake.

### 2.4.4 Kuoanisha Bei ya Maji na Uwezo wa Kulipa

Ikionekana bei ni kubwa au ongezeko la bei ni kubwa ikilinganishwa na uwezo wa wateja kulipa, punguza mapato yanayotegemewa kutoka kwenye bei ya maji mpaka ufikie bei muafaka. Kiasi kitakachopunguzwa kitoke kwenye gharama ya uchakavu na ukarabati'. Vyombo vinapashwa vihakikishe kuwa bei itayopendekezwa inakidhi gharama ya uendeshaji na

matengenezo kwa aslimia 100%.

### 2.4.5 Mapendekezo ya Bei ya Maji

Mapendekezo ya bei ya maji kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Biashara yataainishwa kwa mujibu wa **Jedwali Na: 5** Pia Jedwali hili linatoa fursa ya kulinganisha bei pendekezwa, bei iliyopo na za nyuma yake. Hii husaidia pia kutathmini kama bei pendekezwa imeongezeka sana (Rejea 13.4).

**Jedwali Na. 5: Mapendekezo ya Bei ya Maji**

| **Bei ya Maji** | **M-3** | **M-2** | **M-1** | **Mwaka wa sasa (M)** | **M+1** | **M+2** | **M+3** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Viosk | | | | | | | |
| Majumbani | | | | | | | |
| Taasisi | | | | | | | |
| Biashara | | | | | | | |
| Viwanda | | | | | | | |
| Kurudisha Maji | | | | | | | |
| Viosk | | | | | | | |
| Majumbani | | | | | | | |
| Taasisi | | | | | | | |
| Biashara | | | | | | | |
| Viwanda | | | | | | | |
| Kuunga Maji | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| Jumala ya Gharama za Usambazaji | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| **Bei Nyinginezo** | | | | | | | |

## 3.0 MAPITIO YA MWONGOZO

Mwongozo huu utafanyiwa mapitio kila baada ya miaka mitatu, ama wakati wowote kutakapo jitokeza hitaji la kufanya mapitio hayo kama RUWASA itakavyoona inafaa kufanya mapitio.

Mwongozo huu utatumiwa na Jumuiya za Utoaji wa Huduma ya Maji ngazi ya Jamii.




# Mwongozo Wa Upangaji Bei na Usimamizi wa Makusanyo

RUWASA
Rural Water Supply and Sanitation Agency
"Maji Bombani"

Benki ya NBC,Tawi la Mazengo, Barabara Kuu,
S. L. P 412, 40473 DODOMA.
Simu: +255 2323563/4
Barua Pepe: dg@ruwasa.go.tz